

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**Tamasha la Kimataifa la 37 la Sanaa Na Utamaduni Bagamoyo, Kuanzia Tarehe 20.10.2018-
27.10.2018**

Katika viwanja vya TaSUBa Bagamoyo

TAMASHA la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo litafanyika mjini Bagamoyo kuanzia tarehe 20.10.2018 hadi tarehe 27.10.2018 katika viwanja vya Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa). Tamasha la mwaka huu limebeba kaulimbiu isemayo, "**Sanaa na Utamaduni katika kukuza uzalendo**" - ikiwa ni mahsusi katika kuhamasisha vijana kuipenda nchi yao.

Tamasha la Kimataifa Sanaa na Utamaduni Bagamoyo hufanyika kila mwaka na huandaliwa na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) likiwa na malengo yafuatayo:

- ✓ Kutunza na kuenzi sanaa na utamaduni wa Mtanzania.
- ✓ Kutengeneza jukwaa ambalo wanafunzi wa TaSUBa wanalitumia kupima kiwango chao cha umahiri katika sanaa kwa mwaka katika fani za sanaa za maonyesho na zile za ufundi.
- ✓ Kukutanisha watu wa tamaduni mbalimbali kutoka sehemu mbalimbali za dunia ili kuonyesha utajiri wao wa sanaa na utamaduni.
- ✓ Kutengeneza jukwaa ambalo ni kiungo cha kujenga mahusiano ya wasanii wa ndani na nje ya nchi kupitia maonyesho ya sanaa na pia kubadilishana uzoefu na mawazo katika kuendeleza tasnia ya sanaa.

Mwaka huu Tamasha linafanyika kwa mara ya 37 na litapambwa na ngoma za asili, muziki, sarakasi na maigizo pamoja na maonyesho ya sanaa za ufundi. Pia kutakuwa na warsha na semina zitakazohusu mambo mbalimbali ya kijamii. Jumla ya vikundi vya Sanaa 100 vimethibitisha kushiriki na kati ya hivyo vikundi 10 ni kutoka nje ya nchi (Kenya, Uganda, Zimbabwe, Ivory Coast, Ufaransa, Zambia, Cameroon Ujerumani na Finland).

Ufunguzi rasmi wa Tamasha utafanyika Tarehe 20.10.2018 ambapo mgeni rasmi atakuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mh. Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb); na Ufungaji wa Tamasha utafanyika tarehe 27.10.2018 na mgeni rasmi atakuwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mh. Juliana D. Shonza(Mb).

Mwisho.

Imetolewa na Ofisi ya Habari na Uhusiano (TaSUBa) **16.10.2018**

Mtendaji Mkuu, TaSUBa, S.L.P 32, BAGAMOYO, Tanzania, Simu.: 0255 023 2440149

Barua pepe: bagamoyofest@gmail.com, Tovuti: www.tasuba.ac.tz

Namba za Simu: +255(0) 754 310 425, +255(0) 787 542 242 na +255(0) 655 840 405